# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSIANA NA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

---

**Mheshimiwa Spika,**

Ni wajibu wangu kwa kuanza kumpa nafasi ya kwanza ya shukurani yule aliyenijaalia mimi na nyinyi pumzi na afya na kutuwezesha kuwepo katika ukumbi huu. Naye ni Allah (S.W), mwingi wa utukufu. Naomba kwake aniruzuku pumzi na nguvu ya kuniwezesha kutimiza malengo ya kusimama hapa kuwasilisha Hotuba hii ili nanyi iwafikie kama ilivyokusudiwa. Ni Baraka na furaha kuwasilisha hotuba hii katika Kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani ikiwa bado tupo katika Kumi la pili. Allah atujaalie sote na wananchi wetu tupate fadhila za mwezi huu mtukufu.

Aidha, nachukuwa fursa hii kumuomba Allah (S.W) kwa baraka za mwezi huu atupatie shufaa kutokana na maradhi haya thakili ya **COVID 19** yanayosababishwa na **Virusi vya CORONA**.

Pia, nina wajibu wa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunigaiya muda wako nikaweza kusimama mbele ya hadhara hii ya Waheshimiwa wajumbe wa Baraza kuwasilisha hotuba hii.

Pia, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpa afya njema, nguvu, hekima na busara ya hali ya juu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. ***Dkt. Ali Mohammed Shein***, na kumuwezesha kuwatumikia wananchi katika utumishi uliotukuka zaidi. Zaidi ya hayo nampongeza kiongozi wetu huyo kwa

alivyo mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya Janga la **COVID 19**. Ujumbe wake dhidi ya vita hivyo ni muhimu kuzingatiwa na kila mmoja.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, naomba kumshukuru sana Makamu wa Pili wa Rais, **Mhe. Balozi Seif Ali Iddi** kwa namna anavyotekeleza wajibu wake kama msaidizi nambari moja wa Mheshimiwa Rais.

Aidha, nampongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, **Mhe. Mohammed Aboud Mohammed** na Mhe. Naibu Waziri, **Mhe. Mihayo Juma N'hunga** na watendaji wao wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa utaratibu wa majukumu Wizara hii inasimamia Mafungu ya kibajeti Matano, kama yalivyoainshwa katika kitabu cha Bajeti cha Mhe. Waziri.

Hivyo, ili Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2020/2021**, inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya **Tsh. 75,015,607,000/ (Bilioni Sabiini na Tano, Milioni Kumi na Tano, Laki Sita na Elfu Saba)** ambazo zimetengwa kwa ajili ya shughuli zake za kawaida na Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Bajeti ya Mwaka huu inaonesha utofauti ukilinganisha na Bajeti ya mwaka wa fedha **2019/2020,** Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **48,013,400,000 (bilioni arubaini na nane milioni kumi na tatu na laki nne)** ambazo zilitumika kwa shughuli za kawaida na shilingi **9,897,949,000 (Bilioni Tisa, Milioni Mia Nane na Tisini na Saba, Laki Tisa na Arubaini na Tisa Elfu)** kwa Miradi ya Maendeleo. Kamati imeridhika na utekelezaji wa Bajeti katika mwaka wa fedha **2019/2020**.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, kwa mwaka wa fedha **2020/2021,** Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi TZS. **232,500,000/ (Milioni Mia Mbili na Thelathini na Mbili na Laki Tano)** kutoka vyanzo mbali mbali katika Wizara hiyo. Hata hivyo, Kamati imebini kuwepo kwa tofauti kubwa ya makadirio ya mapato yatakayokusanywa kupitia vyanzo mbali mbali katika mwaka wa fedha 2020/2021 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020, ambapo jumla ya shilingi TZS **304,410,000 (Milioni Mia Tatu na Nne, Laki Nne na Efu Kumi)** zilitarajiwa kukusanywa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilitarajia kuona uwepo wa ongezo la mapato yatakayokusanywa katika mwaka wa fedha 2020/2021, kutokana na kuwepo kwa viashiria mbali mbali vya ukusanyaji wa mapato kupitia taasisi mbalimbali katika Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo, Kamati inashauri Taasisi za ukusanyaji wa mapato katika Wizara hiyo kusimamia vyema ukusanyaji huo wa Mapato kupitia vyanzo walivyonavyo ili kuona malengo ya Wizara na Serikali yanafikiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ujumla shughuli zote za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha **2020/2021,** zitakuwa na **Mafungu Ma**kuu matano, ambayo ni **Fungu C01-** Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais**, Fungu CO2-** Baraza la Wawaklishi, **Fungu C03-** Tume ya Uchaguzi, **Fungu C04-** Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti Dawa ya Kulevya, na **Fungu C05-**Tume ya Ukimwi. Mafungu hayo yote yatatekelezwa kupitia Programu Kuu pamoja na Programu Ndogo.

**Mheshimiwa Spika;**

Baada ya kueleza Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili kwa ujumla, sasa kwa idhini yako naomba nitoe maoni ya Kamati yangu, ambayo yatajikita kwa kila Taasisi kwa mujibu wa Programu, shughuli na huduma zilizopangwa kutekelezwa, ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Makamu wa Pili imepanga kutekeleza Programu Kuu kumi na moja (11) na Programu ndogo ishirini na tano (25) kama ifuatavyo:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (C01)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imepitia na kuridhia jumla ya fedha zote zinazokusudia kutekeleza jumla ya Programu kuu tatu (3), katika fungu la C01, nazo ni:

1. Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais,
2. Uratibu wa Shughuli za Serikali, na
3. Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais.

Lengo la Programu Kuu zote tatu ni pamoja na kuimarisha utendaji wa kazi wa Ofisi ya faragha ya Makamu wa Pili.

**Mheshimwa Spika,**

**Programu ya Uratibu wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais**

Katika Programu Kuu hii, Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushughulikia malalamiko 29 ya wananchi yaliyowasilishwa na kuyapatia ufumbuzi malalamiko 20. Aidha ofisi inaendelea kufuatilia utatuzi wa malalamiko yaliobakia. Kamati imefurahishwa na utatuzi wa migogoro, ni matumaini yetu migogoro iliyobaki itapatiwa ufumbuzi haraka iwezekanavyo.

**Mheshimwa Spika,**

Kwa ujumla Kamati imeridhika na matengenezo yaliyofanywa katika nyumba za Makumu wa Pili wa Rais, Mazizini Unguja, Dar es Salam na Dodoma kwa mwaka wa fedha 2019/2020**,** pamoja na kusimamia uteklezaji wa ahadi 14 zilizotolewa na Makamu wa Pili wa Rais kwa wananchi mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo; Kamati ilitarajia kuona kuwepo kwa mpango wa ujenzi katika eneo la Dodoma ambalo Ofisi ya Makamu wa pili imekabidhiwa kwa ajili ya Ofisi za SMZ Dodoma. Kukosekana kwa mpango huo katika Bajeti hii kunaashiria kumaliza kwa awamu ya saba bila kuanza hatua za awali za ujenzi Dodoma jambo ambalo Kamati hikulitarajia.

**Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu kuu hii ina Programu ndogo saba zifuatazo:

1) Programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa,
2) Programu ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
3) Programu ndogo ya Shughuli za SMZ,
4) Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar-Dar-es-Salaam,
5) Programu ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu,
6) Programu ndogo ya Usimamizi wa Mazingira,
7) Programu ndogo yaUratibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

**Programu ndogo ya kukabiliana na maafa**

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo la progrmamu hii ni kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa kabla, wakati na baada ya kutokea Programu hii inasimamiwa na Kamisheni ya kukabiliana na maafa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamisheni imepanga kutekeleza shughuli mbali mbali kama zilivyoainishwa katika kitabu cha Bajeti ya Wizara. Miongoni mwa shughuli hizo ni kuandaa miongozo itakayosaidia kuratibu shughuli za kukabiliana na majanga hapa Zanzibar pamoja na Kuandaa mfumo jumuishi wa kuhifadhi taarifa za maafa hapa Zanzibar. Aidha; Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya matukio ya majanga nalo limepewa nafasi yake.

Shughuli nyingine iliyopangwa kufanywa ni ukaguzi katika maeneo mbali mbali kwa dhamira ya kuangalia uwepo wa mipango na taratibu za kukabiliana na maafa kwa Unguja na Pemba.

Kwa ujumla Kamati inaipongeza Kamisheni kwa namna ilivyojipanga katika kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa bado jamii haijakubali kupokea mwitiko wa masuala ya maafa na ndiyo maana hadi sasa watu wanaoishi katika maeneo hatarishi wanaendelea kubaki katika maeneo hayo licha ya maafa wanayopata kila zinaponyesha mvua. Kamati inaisisitiza Kamisherni kulichukulia hatua stahiki suala hilo.

**Programu ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ndogo ndio yenye dhamana ya Kusimamia Sherehe za Kitaifa na Maadhimisho sambamba na kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa**.**

Kamati imeridhishwa na utendaji wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia programu hii kwa kutekeleza majukumu yao vizuri.

Kamati inapongeza namna sherehe za mapinduzi ya Zanzibar ya 1964 ambayo hufanyika kila ifikapo tarehe 12 Januari inavyopewa uzito unaostahiki.

Aidha, Uratibu wa Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na shughuli za kuwaenzi viongozi nazo zinafanywa kwa umahiri mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapongeza kwa dhati Idara ya sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kwa kupanga katika mpango kazi kwa Bajeti ya mwaka 2020/2021, kumalizia ujenzi katika jengo la Ofisi hiyo liliopo Mwanakwerekwe.

**Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

**Mheshimiwa Spika,**

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepanga kutekeleza shughuli mbali mbali, Miongoni mwa shughuli hizo ni Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na kutoa taarifa za utekelezaji wa Ilani kwa Wananchi. Sambamba na hilo idara hii pia husimamia utekelezaji wa ahadi za Viongozi wakuu wa Kitaifa na kuandaa taarifa ya Utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Idara hii pia ndiyo yenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imepanga shughuli kadhaa kama vile Kuratibu na kusimamia malipo kwa kaya masikini katika Shehia za Unguja na Pemba. Kusimamia uendeshaji wa Shughuli za TASAF kwa Unguja na Pemba;

Kamati inaipongeza Idara kwa kazi nzuri inayofanya katika kusimamia miradi ya TASAF. Hata hivyo Kamati inasisitiza kwamba suala la matumizi ya fedha kwa miradi hiyo lisimamiwe ipasavyo. Aidha, Idara ihakikishe inasaidia walengwa kuibua miradi yanye tija na endelevu. Hivyo walengwa waweze kupatiwa elimu juu ya uibuwaji wa miradi hiyo na kufikia malengo.

Sambamba na Idara kuhakikisha kuwa inamjumuisha kila anayestahiki kuwemo katika miradi hiyo na hakuna atakayeachwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Jumla ya shilingi TZS 21,597,995,338 **(Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Tano na Tisiini na Saba, Laki Tisa na Eflu Tisini na Tano, Mia Tatu na Thelathini na Nane)** zimetengwa kwa mradi huo ambazo ni mchango wa Serikali na Washirika wa Maendeleo.

**Programu Ndogo ya Usimamizi wa Mazingira na Programu ndogo ya Uratibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo la programu kuu hiyo ni kuhakikisha usimamizi endelevu wa masuala ya kimazingira. Kamati imeridhishwa na kazi zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii kwa mwaka wa fedha **2020/2021.**

Miongoni mwa kazi hizo ni Kutayarisha Kanuni za Mazingira zinazotokana na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2015, Kuendesha na kusimamia operesheni za

kusimamia upigaji marufuku ya mifuko ya plastiki na za kusimamia maliasili zisizorejesheka na kutoa elimu kwa jamii ya uhifadhi wa mazingira kupitia vipindi vya Redio na Televisheni.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa uratibu wa mazingiza na mabadiliko ya Tabia nchi, Kamati imefurahishwa na jitihada za Idara katika kulinusuru eneo la Msuka Pemba lililoathiriwa na Mabadiliko ya Tabianchi.

Suala la kuandaa maandiko ya miradi inayohusiana na mabadiliko ya tabianchi kupitia Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Fedha za Mabadiliko ya Tabianchi ni jambo muhimu na la kupongezwa. Kamati inasisitiza kuwa kabla ya kuandika miradi hiyo Idara inatakiwa kufanya utafiti wa kutosha kuhusiana na tatizo hilo ili waweze kuandika huku wakiwa na taarifa za uhakika na zenye kujitosheleza. Ni imani ya Kamati kuwa miradi hiyo inaweza kuwa ni suluhisho la tatizo la athari za tabia nchi. Miongoni mwa maeneo yaliyoathirika na athari za tabia nchi ni kisiwa cha Mnemba ambacho ni kisiwa kinachoingiza mapato makubwa kupitia utalii na kuonekana kila siku kinaendelea kupungua. Hivyo Kamati inashauri Idara kulitumia eneo hilo kuwa miongoni mwa maeneo ya utafiti.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Programu hii Idara ya Mazingira, inategemea kutumia **Shilingi 1,265,712,000 (Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Sitini na Tano, Laki Saba na Elfu Kumi na Mbili)** kwa kazi za maendeleo zikiwa ni mchango wa Serikali na Washirika wa Maendeleo ambao ni UNDP na ADB**.**

Kamati inasisitiza Idara kuendelea kusimamia vyema fedha za Miradi ya Maendeleo ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar-Dar-es-Salaam**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ina lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya Taasisi/Wizara za SMZ na SMT, Washirika wa Maendeleo, Ofisi za Kibalozi na asasi nyengine za kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa mambo yaliyokusudiwa kutekelezwa kupitia Programu hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ni kuratibu shughuli za kisekta za Wizara na Taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kufuatilia masuala mbalimbali

yanayohusu Wizara na Taasisi za SMZ kwa Taasisi za SMT, Ofisi za Kibalozi na Mashirika ya Kimataifa.

Aidha, suala la kutoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Watendaji wengine wa SMZ wanapokuwa Tanzania Bara ikiwemo mapokezi, usafiri na uratibu wa upatikanaji Viza.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utendaji wa Ofisi ya SMZ Dar es salaam na inaipongeza kwa kazi nzuri.

**Programu Ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo ya usimamizi wa masuala ya Watu wenye Ulemavu lengo lake kuu ni kuhakikisha ujumuishwaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu unafanyika katika ngazi zote. Kazi za Programu hii zinatekelezwa na Idara ya Watu wenye Ulemavu.

Miongoni mwa mambo ya msingi yanayokusudiwa kutekelezwa kupitia programu hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ni kufanya tafiti mbili (2) juu ya vikwazo vya kielimu vinavyowakumba Watu wenye Ulemavu na tathmini ya elimu mjumuisho kwa Watu wenye Ulemavu Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Suala la kufanya utafiti uliotajwa hapo juu ni muhimu sana kwani ukweli ni kwamba watu wenye ulemavu wanachangamoto kubwa katika kufikia malengo ya kupata haki yao ya kikatiba ya kupata elimu ambayo ni ya kila mmoja wetu. Wenzetu wenye ulemavu wamekuwa wakikumbwa na changamoto tokea za upatikanaji wa vifaa vya kifundishia na kujifunza, uhaba wa walimu wenye sifa, miundo mbinu rafiki na mengi mengine. "***Tunapaswa tukumbuke kuwa kila mmoja wetu ni mlemavu mtarajiwa"***

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo ni matumaini ya Kamati kwamba utafiti huo utasaidi kuainisha changamoto hizo na namna ya utatuzi wake.

Kamati inaitaka Idara kushirikiana kikamilifu na washirika wengine hasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kuhakikisha kwamba utafiti huo unazaa matunda yanayotarajiwa.

Aidha suala la Kuimarisha fursa za Watu wenye ulemavu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye ulemavu Zanzibar nalo ni jambo la kupongezwa.

Kamati inashauri kwamba ili watu wenye ulemavu waweze kuzifikia fursa hizo sauala la kuwapatia elimu juu ya fursa husika ni muhimu.

**BARAZA LA WAWAKILISHI (C02)**

**Mheshimiwa Spika,**

Baraza la Wawakilishi linatekeleza Programu kuu mbili ambazo ni Programu Kuu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali na Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatelekelezwa Zanzibar na kwa upande wa Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,**

kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, miongoni mwa mambo yaliyopangwa kutekelezwa na Baraza la Wawakilishi ni kujenga mazingira mazuri kwa kuwezesha kufanyika kwa vikao vya Baraza la Wawakilishi pamoja na kazi za Kamati, Kutoa mafunzo kwa ajili ya kuwaongezea uwezo wa kitaalamu Wajumbe na Wafanyakazi wa Baraza na kutoa taaluma kwa wananchi kuhusu utendaji wa shughuli za Baraza kupitia vyombo vya habari.

**TUME YA UCHAGUZI (C03)**

**Mheshimiwa Spika**,

Programu hii ina jukumu la kuimarisha usimamizi wa mwenendo wa shughuli za uchaguzi, ambayo matarajio yake ya muda mrefu ni uendeshaji bora wa kazi za Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, miongoni mwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kupitia Programu hii ni Kuimarisha majengo ya Ofisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Kutoa elimu ya Uchaguzi kwa Wajumbe na Watendaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Kuendelea kutoa fursa za kujiendeleza kitaaluma kwa wafanyakazi katika ngazi mbali mbali za elimu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi Mkuu ni matumaini ya Kamati kuwa Tume ya uchaguzi imejipanga ipasavyo kukabiliana na zoezi hilo kwa upande wa vitendea kazi pamoja na rasilimali watu ili kuhakikisha kwamba kila mwenye sifa anapata haki yake ya kushiriki katika uchaguzi na kupelekea kuimarisha demokrasia ya kweli Zanzibar.

**TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI DAWA YA KULEVYA (CO4)**

**Mheshimiwa Spika,**

Fungu C04 lina jumla ya Programu Kuu mbili. Programu ya udhibiti wa dawa za kulevya na programu ya uendeshaji na uratibu wa dawa za kulevya ambazo zina programu ndogo nne.

**Mheshimiwa Spika,**

Jukumu kuu la Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ni kuratibu mapambano dhidi ya biashara, usafirishaji na matumizi ya Dawa za Kulevya kwa kutoa taaluma kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya, tiba na ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya miongoni mwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na Kuanzisha Kituo cha Huduma za Pamoja cha Uendeshaji wa kesi za Dawa za Kulevya (One Stop Centre).

**Mheshimwa Spika,**

Suala la mapambano ya Dawa za kulevya ni la kila mmoja wetu na linahitaji nguvu ya pamoja, hivyo kuwa na kituo cha aina hii ni jambo jema sana na Kamati inaamini suala la mkwamo wa kesi hizo utakuwa umepata ufumbuzi.

Kuhusu Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni; Kamati inapongeza hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa kituo hicho. Hata hivyo, Kamati inaamini kwamba mradi huo utakuwa unafikia mwisho katika Bajeti hii kwani mradi ni wa muda mrefu.

Kwa upande wa suala la Kuteketeza Dawa za Kulevya zilizohifadhiwa kisheria ni jambo muhimu na linalopaswa kupewa uzito unaostahiki. Tume ihakikishe kuwa kuna udhibiti wa kutosha katika kutekeleza suala hilo.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya kazi nzuri na ya kupongezwa inayofanywa na Tume ya kudhibiti dawa za kulevya Kamati imebaini kuwa bado kuna mianya ya upitishaji wa Dawa hizo haramu hasa kupitia madiko na Bandari zisizo rasmi.

Kamati inashauri kwamba katika mwaka wa fedha 2020/2021, katika Mapambano dhidi ya dawa za kulevya kuweka mkazo zaidi katika kudhibiti Madiko na Bandari zisizo rasmi kwa kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo kwa mashirikiano ya wadau wote muhimu.

**TUME YA UKIMWI (C05)**

**Mheshimiwa Spika**,

Fungu **C05** lina program kuu mbili, Programu ya kuratibu mwitiko wa Taifa wa UKIMWI na Progrmu ya utawala na uendeshaji. Aidha, program ndogo nne zipo chini ya Programu kuu hizo.

**Mheshimiwa Spika**,

Kimsingi, Tume ya UKIMWI ya Zanzibar ina jukumu la kuratibu na kuongoza mapambano ya Kitaifa dhidi ya UKIMWI ambayo yanajumuisha sekta zote nchini ambapo inatekeleza majukumu yake kupitia Programu nilizozitaja hapo juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Tume imepanga kutelekeza shughuli mbali mbali, miongoni mwa hizo ni Kufanya mikutano ya uratibu wa Taasisi za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia na Taasisi za kidini, Kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuratibu muitiko wa jamii wa UKIMWI na Kuongezea uwezo mfumo wa ufuatiliaji wa Programu za UKIMWI kwa kutoa mafunzo na kufanya ukaguzi wa taarifa ili kutoa ripoti sahihi za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya kwamba maradhi ya UKIMWI kwa sasa yanaonekena kama ni maradhi ya kawaida lakini bado jamii inapaswa kuelewa kuwa ni maradhi hatari na yanaathiri nguvu kazi. Hivyo Tume ya UKIMWI bado inajukumu kubwa la kushughulika na jamii na kufanya tathmini ya mwitiko wa UKIMWI kwa jamii.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**,

Kwa kumalizia maoni haya ya Kamati kwa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa mwaka wa **fedha 2020/2021**, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika bila ya

kumsahau Katibu wa Baraza la Wawakilishi**,** kwa kuwa nami pamoja na Kamati yangu bega kwa bega, mara zote tunapohitaji ushauri na muongozo wenu. Aidha niwashukuru pia watendaji wote wa Afisi ya Baraza, kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kutoa huduma kwa Waheshimiwa Wajumbe ili kuhakikisha Baraza linatekeleza kazi zake kwa ufanisi.

Shukurani zangu za pekee ziwaendelee Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa kuonesha ushirikiano na uvumilivu, katika kazi zetu za kuisimamia Serikali ndani ya kipindi chote cha mwaka wa fedha **2019/2020**. ni matumaini yangu kuwa, katika kipindi chote hichi, Wajumbe wamejifunza mengi na kutegemea ufanisi zaidi katika mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ruhusa na idhini yako, naomba niwatambue Wajumbe wote wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Panya Ali Abdalla — Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) — M/Mwenyekti
3. Mhe. Viwe Khamis Abdalla — Mjumbe
4. Mhe. Ame Haji Ali — Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu — Mjumbe
6. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame — Mjumbe
7. Mhe. Rashid Ali Juma — Mjumbe

Bila kuwasahau Makatibu wetu wawili ambao ni:

1. Ndg. Karima Abdul Wahab — Katibu, na
2. Ndg. Talib Enzi Talib — Katibu.

**Mheshimiwa Spika:**

Naomba kulidhihirishia Baraza lako kuwa Wajumbe wachapakazi, weledi na wenye uzalendo wa hali ya juu wa katika Kamati hii sambamba na wasaidiszi wao yaani Makatibu ambao wamewezesha kuipitia, kuichambua na kuitolea maoni bajeti hii katika maeneo mbali mbali hatimae kujiridhisha. Hivyo Kamati imekubaliana na Bajeti Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha **2020/2021**.

**Mheshimiwa Spika**,

Baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

……………………………
Panya Ali Abdalla,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.
Baraza La Wawakilishi
**Zanzibar**